Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 79 No. 202 | JAM. II-RAJAB 1439 AH | MACHI 2019 | AMMAN 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Sema, " Je Tuwaambieni wale wenye hasara zaidi kuhusiana na vitendo vyao?

Ni ambao bidii yao imepotea katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanazifanya vema sana.

(Al Kahf 18:104-105)

Fanya Biashara, Achana na Riba



Makala uk 9

Khuddamul Ahmadiyya Waadhimisha Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

Na **Mwandishi Wetu**



Jumapili ya tarehe 17 Februari 2019 Khuddamul Ahmadiyya Tanzania walizunguuka kwa baiskeli katikati ya mitaa ya jiji la Dar es salaam wakigawa vipeperushi vya Jamaat na kuzitoa takbira. Tukio lilifanyika Jumapili siku chache kabla ya 20 Februari – Siku ya Mwana Aliyeahidiwa katika kalenda yetu ili kuutumia vyema utulivu wa mitaa, na pia kuleta mwamko juu ya tukio hili miongoni mwa Atfal na Khuddam kabla ya siku rasmi ya maadhimisho.

Takriban Khuddam na Atfal 150 walizunguuka na baiskeli kwa saa mbili wakiongozwa na Sadr Majlis Bw. Ramadhani Nauja. Tukio limehudhuriwa na Amir Jamaat Tanzania Maulana Tahir Mahmood Chaudhry, Naibu Amir Ndugu Issa Andendikisye Mwakitalima, Naibu Amir Tabligh na Tarbiyyat Sheikh Bakri Abedi Kaluta na mwakilishi kutoka Ofisi

Endelea uk. 9

Wasabato Masjid Salaam

Na **Mwandishi Wetu**



Katika tukio la aina yake lilitokea siku ya Ijumaa ya tarehe 8 Machi 2019, Masjid Salaam mahali palipo makao makuu ya Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya nchini Tanzania, walikaribishwa ndugu zetu Wakristo wa madhehebu ya Wasabato na kushuhudia sala ya Ijumaa na kupata fursa ya kujionea na kujifunza mambo mbalimbali ya dini ya Islam.

Wakiongozwa na Mchungaji Steven Ngusa ambaye ni Askofu Mkuu wa jimbo la Kusini Mashariki mwa Tanzania, Mchungaji Dominick Pius Mapima ambaye ni mratibu wa mahusiano ya kidini wa jimbo la Kusini Mashariki mwa Tanzania na Mchungaji Wilfred Mafwimbo ambaye ni Katibu Mkuu wa jimbo hilo la Kusini Mashariki mwa Tanzania, walipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ya msikiti na kupata maelekezo ya kina kutoka kwa Katibu wa Tabligh Ally Mbambwa Sahib.

Endelea uk. 2

Tumia Chombo Hiki Usalimike Uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

QUR'AN TUKUFU KWA KISWAHILI

Kuna haja ya kuyaweka baadhi ya mambo sawa katika historia. Ipo hatari ya kufikiri mambo yalikuwa mteremko wa Salanda. La hasha! Mambo hayakuwa hivyo.

Kuna wakati katika historia yetu fikira tu ya kwamba unaweza kutafsiri Qur'an tukufu lilikuwa ni kosa ambalo hukutakiwa kusamehewa. Haiwezekani. Ni ukafiri. Wewe uliona tangu lini. Wingu hilo la fikra potofu liliondolewa na askari wa Masihi Aliyeahidiwa[as], Sheikh Mubarak Ahmad ambaye mwaka 1953 alitoa tafsiri bulbul na tamu ya Qur'an Tukufu katika lugha yetu adhimu. Kumbe Kiswahili kina uwezo na makamu ya kubeba ujumbe mzito uliomo katika sharia ya mwisho kwa binadamu. Alhamdulilah. Tongo tongo zilizokuwa zimetujaa machoni zikatoka na maneno ya Allah tukayaelewa katika lugha yetu.

Sheikh Mubarak Ahmad alifungua njia na kwa hivi sasa tunazo tafsiri nyingi katika lugha ya Kiswahili. Mwiko umekwishaondolewa na juhudi zinaendelea za kuwa na tafsiri nyingi zaidi za Qur'an Tukufu katika Kiswahili.

Wakati tunafurahia na kusherehekea tafsiri nyingi za Qur'an Tukufu katika Kiswahili tunakabiliwa na suala moja la msingi, je tumepata uwezo wa kugusa maana za ndani za Qur'an Tukufu? Je, kwa nguvu zetu, uwezo wetu, ujanja wetu tunaweza kuzifikia maana za ndani za Qur'an Tukufu? Jibu letu ni kwamba hiyo si kazi rahisi. Na hoja yetu ya msingi ni kwamba kutokana na uzito wa ujumbe uliomo katika Qur'an Tukufu, Allah Alimteua Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] kutueleza maana za ndani za Qur'an tukufu. Kwa uwezo wa Allah Masihi Aliyeahidiwa[as] amefafanua na kueleza kwa ufasaha falsafa nzima ya Qur'an Tukufu. Hakuna anayeweza kuielewa Qur'an Tukufu bila kunywa kutoka katika chemchem aliyopewa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Vitabu takriban 80 vimeandikwa kwa madhumuni hayo hayo ya kueleza maana za ndani za Qur'an Tukufu. Kazi hii yenye taadhima imeendelezwa na Makhalifa wa Masihi Aliyeahidiwa[as] ambao wameendelea kutoa majibu ya matatizo yetu yote kutoka kwenye Qur'an Tukufu.

Mwanzoni mwa miaka ya 30 wazo la kutafsiri Qur'an Tukufu lilitupiliwa mbali na maulamaa wa enzi hizo. Hivi sasa sio tu kwamba Qur'an Tukufu inatafsiriwa katika Kiswahili, bali kuna mashindano ya kuitafsiri katika Kiswahili. Ni jambo jema kushindana katika wema. Hoja yetu ambayo tunaomba muiweke maanani ni kwamba yeyote anayetaka kupata maana za ndani za Qur'an Tukufu hana budi kufunga safari na kumuendea Masihi Aliyeahidiwa[as]. Kazi hii amepewa na Allah na anayetaka kutuliza kiu yake aje na vyombo vyake ili ajichotee maji ya kutosha ya kukata kiu au sivyo atabaki nje akinywa maji ya chumvi ambayo dawamu hayakati kiu bali yanaongeza kiu.

Wasabato Watembelea Masjid Salaam

Kutoka uk. 1

Akiwakaribisha msikitini hapo wakati wa Sala ya Ijumaa mtoa hotuba Chaudhry ambaye alitumia muda wake kuwashukuru wageni majibu, ambapo walitaka kujua msimamo wa Ahmadiyya juu ya Issa Bin Mariamu, tofauti baina ya Ahmadiyya na Waislam wengine, na maana ya Kiama. Majibu ya kina na fasaha yalitolewa na Sheikh Abdulrahman Ame na mmoja wa wageni alisikika akisema namna alivyomuelezea Issa Bin Mariamu hakika Sheikh Ame ni "msabato". Mgeni mwingine alivutiwa na elimu aliyopata juu ya mchango wa mfalme Mkristo alivyowasaidia Waislam wa mwanzo hakika anahitaji hotuba za namna hiyo zinazoonyesha uhusiano mwema baina ya dini hizi mbili kuwa ni siku nyingi sana.



Amir na Mbashiri Mkuu akiongea na Wasabato walipotembelea Masjid Salaam

Sheikh Abdulrahman Ame alieleza uhusiano uliopo baina ya Waislam na Wakristo ulianzia wakati wafuasi wa Mtume Muhammad[saw] alipowaelekeza waende Ethiopia nchi ambayo mfalme wake alikuwa Mkristo ili wakapate fursa ya kufanya ibada na kuishi kwa amani. Pamoja na fitna toka kwa maadui bado Mfalme Mkristo muadilifu hakutoa nafasi ya maadui kuwadhuru Waislam katika ardhi yake. Aidha alikumbusha pia jinsi Mtume Muhammad[saw] alivyowakaribisha Wakristo msikitini na kufanya nao mazungumzo na ulipofika wakati wa sala walipata nafasi ya wao kufanya ibada kwani msikiti ni mali ya Allah hivyo kila mtu anayeabudu Allah ana haki ya kuutumia bila ya kufanya fujo na uharibifu. Ndugu zetu hao ambao walifika kabla ya sala ya Ijumaa na kushuhudia taratibu zote za ibada kwa macho yao wakiwa wameketi kwenye viti, walikuja pia na akina mama ambao walikuwa upande wa Lajna.

Baada ya sala ya Ijumaa, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania Seif Hassan Nakuchima Sahib aliwatambulisha baadhi ya viongozi wa Jamaat waliokuwepo kuwapokea wageni na kumkaribisha Amir Sahib Sheikh Tahir Mahmood kwa kuja na kutembelea msikiti na kujifunza imani ya Islam Ahmadiyya. Amir Sahib alitoa historia ya Ahmadiyya duniani na kuelekeza kidogo misukosuko tunayoipata katika baadhi ya nchi hapa duniani kwa sababu ya kukosa uvumilivu wa imani tofauti na kupigia mfano wa nchi ya Pakistani.

Aidha wageni wetu walitoa zawadi ya vitabu mbalimbali kwa Amir Jamaat na kupata neno la shukran kutoka kwa Katibu Mkuu wa jimbo Ndg, Wilfred Mafwimbo ambaye alikiri hii ni mara yake ya kwanza kuingia msikitini na hawakutarajia mapokezi mema na ukarimu walioupata kutoka Ahmadiyya na alitumia fursa hiyo pia kuwakaribisha Wanajumuiya ya Ahmadiyya katika Mkutano wa amani uliuoandaliwa na Kanisa la Wasabato jimbo la Kusini Mashariki mwa Tanzania utakaofanyika siku ya Jumapili pale Temeke.

Mwishowe ilipatikana fursa ya maswali na

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Historia ya Jamaat Pwani

Na

Mwl Nassoro

Hussein,

Pwani



Kwa maelezo ya Muheshimiwa Amiri Sahib ameelekeza ya kwamba iandikwe historia fupi ya jinsi Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya ilivyobisha hodi kwa mara ya kwanza mkoa wa Pwani. Hapa ifahamike kuwa, kuandika historia, inayohusu jambo lolote lililotendeka· miongo mingi iliyopita huwa si jambo jepesi. Hivyo inahitajika wapatikane watu waliopata kuona au kusikia, pindi jambo fulani lilipofanyika, kwenye nyakati hizo, ambapo kizazi cha leo kilikuwa bado hakijapatikana hapa Duniani. Hivyo basi ili kupata historia inayoeleza, kwa namna gani na mwaka gani Jamaati Ahmadiyya ilivyoingia mkoani Pwani, imenipasa niwatembelee baadhi ya wazee wa Jumuiya, waliojiunga na Jamaati mapema kabisa wakati Jamaati inaingia mkoani humu. Mzee Uwesu Sozigwa, ni Mzee anayepindukia umri wa miaka 88 hadi sasa. Kwa namna ya pekee ameweza kunisaidia kupata baadhi ya maelezo, yanayofanya niweze kuandika historia ya Jamaati mkoani Pwani. Mzee Sozigwa anasimulia ya kwamba Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya iliingia mkoa wa Pwani kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1952.

Ikianzia Rusende Nyipara Wilayani Rufiji ni katika mwaka huo. Maulana Sheikh wetu Marehemu, Shekhe Swalehe Mbarouk, Kapilima Lihomba alifika Rusende huko Nyipara kwa ajili ya Mahubiri. Inaelezwa ya kwamba Shekhe Swalehe, alipofika Nyipara hakujionyesha kwamba yeye ni Ahmadiyya, bali alijichanganya na wenyeji katika mambo yote, hata inasemeka alipata kuoa Mke wa Kirufiji alipokuwa hapo Nyipara na kwa vile alikuwa na ujuzi wa Elimu ya Dini akapata kufungua Madrasa (Chuo) kwa ajili ya kufundisha masomo ya Dini. Madrasa hiyo ikapata mafanikio makubwa, Watoto hata watu wazima, kina Baba, akina Mama, wote kwa pamoja, wakawa wanasoma katika Chuo hicho. Hapo Shekhe Swalehe akapata umaarufu mkubwa, wenyeji wakamwamini, kwa mambo mengi. Hata aliweza kualikwa kwenye shughuli mbalimbali za kidini kama vile Kalamu, Arobaini, Malimati n.k. lakini ifahamike hapa ya kwamba, japo Shekhe alikuwa akienda kwenye shuguli hizo, hakupata kula chakula kilichopikwa kwa



Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima

niaba ya shughuli hizo. Na mara zote alipoulizwa ni kwa nini bali vyakula kwenye Hitima au Kalamu, alikuwa akiwajibu kwamba nitawaambieni siku nyingine, "anasimulia mzee Sozigwa." Ikatokea siku moja alipokuwa akifundisha Madrasa, Shekhe Swalehe aliwaambia Wanafunzi kwamba mambo ya Kalamu, Arobaini n.k. sio mambo ya Kiislamu, huku akitoa ushuhuda ndani ya Qurani na hadithi mbalimbali za Mtume mtukufu*saw* kuhusiana na ubovu wa mambo hayo.

Waahmadiyya walitengwa hadi kwenye Visima vya Maji, ilikuwa ikitutokea tu Mwanajamaati katumia Kata au Kikombe kunywea Maji, akionekana na mtu asiye Mwanajamaati basi Kata ile huvunjwa, na kama ni Kikombe, kilitakiwa kioshwe mara saba kwa Mchanga, na dua ya kutakasa isomwe.

Na kwa vile wenyeji wake ulipofeli, wapinzani wakaenda walikuwa wamemkubali na kumuamini, wengi miongoni mwao waliachana na itikadi hizo. Ni katika kipindi hicho pole pole kwa hekima kubwa kidogo kidogo, Shekhe Swalehe alianza kuhubiri habari za ujio wa Masihi Aliyeahidiwa na Imamu Mahdi. Katika Mahubiri yake hayo Shekhe aliwavuta wengi miongoni mwa Wananyipara, kwa kuwa mahubiri yake yalikuwa na ushahidi wa Qurani tukufu na Hadithi za Mtume*saw* hapo ndugu wengi, wakajiunga na Jumuiyya kupitia mahubiri hayo, watu zaidi ya 216 kwa mpigo wakajiunga na Jamaati Ahmadiyya, wakiwemo kina Baba na kina Mama, Vijana kwa Wasichana.

Changamoto Zinaanza Baada Ya Kujiunga Na Jamaat

Kwa mujibu wa masimulizi ya Mzee Uwesu Sozigwa anasimulia ya kwamba, baada ya wao kujiunga na Jamaati Ahamadiyya, walikabiliana na changamoto za namna mbalimbali hasahasa chuki. Wanajumuiya walichukiwa sana kiasi kwamba kama ilitokea Mwanachama wa Jamaati kugusa tu nazi Sokoni, ilionekana nazi hizo ni najisi, Waahmadiyya walitengwa hadi kwenye Visima vya Maji, ilikuwa ikitutokea tu Mwanajamaati katumia Kata au Kikombe kunywea Maji, akionekana na mtu asiye Mwanajamaati basi Kata ile huvunjwa, na kama ni Kikombe, kilitakiwa kioshwe mara saba kwa Mchanga, na dua ya kutakasa isomwe. Katika mkondo huo wa chuki, kukazuka fitina kubwa ya kukata udugu na hata kuvunjiana Ndoa, Nyumba za Wanajamaati ilihukumiwa zichomwe Moto nyakati za usiku, Mungu alisimama upande wa Wanajamaati kwa kuivunja njama ile. Kulipokucha asubuhi mmoja miongoni mwa maadui, akavujisha siri, kwa baadhi ya Wanajamaati, kwa kuwaambia ya kwamba, usiku wa jana kuamkia leo tulikuja ili kuzichoma Nyumba zenu, lakini tulishangaa kuona kana kwamba Nyumba zenu zipo kwenye Kisiwa cha Bahari hivyo tulishindwa kukufikieni, na hatimaye tuliamua kurudi. Mpango huo kushitaki Mahakamani kwa ajili ya nia yao. Hivyo waliteuliwa baadhi ya Wazee maarufu kwa ajili ya kupeleka mashtaka Bomani.

Waahmadiyya Waitwa Kortini Utete

Bw John Yange ndiye aliyekuwa D.C. wa Rufiji wakati ule wa Ukoloni, aliwapokea wajumbe hao na akawasikiliza malalamiko yao dhidi ya Wanajamaati, na Jumuiya kwa ujumla. Hivyo Bw. John Yange D.C. aliwaandikia Wanajamaati wito wa Mahakama (samans) kwa ajili ya kwenda kujibu mashtaka yanayo wakabili siku ilifika ya pande zote mbili kufika Mahakamni. D.C. aliwaambia Viongozi wa suni, watoe mashtaka yao dhidi ya Waahmadiyya. Mashekhe katika malalamiko yao walimweleza D.C. ya kwamba, Waahmadiyya wameleta Dini mpya, inayopotosha watu. Bw D.C. Yange aliposikia hivyo, alitaka kusikia kutoka upande wa Jumuiya, dhidi ya mashtaka yanayowakabili Shekhe Swalehe Mbaruku, wakati huo ndiye aliyekuwa mbashiri wa kujitegemea Nyipara. Aliieleza Mahakama itikadi na Imani za Waahmadiya, katika Islam. Kisha kiongozi wa Masuni alisimamishwa ili ajibu hoja za upande wa Jamaati, Shekhe alishindwa mbele ya Mahakama, kwa kueleza maelezo ambayo yalikuwa nje ya mada. Muheshimiwa D.C. alijitahidi sana kumrai Shekhe ili arudi kwenye mada ikashindiakana, badala yake akaanza kupayuka kwa kusema hawa dawa yao ni kuwa nyang'anya wake, na kuwafukuza Kijijini kwetu. D.C. akamjibu, kazi ya Mahakama si kuvuja Ndoa za watu, wala kufukuza watu katika Miji yao. Hapo D.C. Yange akaamuru ya kwamba Wanajaamati wasisumbuliwe tena. Masuni wakaanza kulalamika eti D.C. amependelea wa Ahmadiyya.

Wapinzani Wageukia Nguvu za Giza

Wapinzani walipoona kuwa wameshindwa vibaya pale Utete Mahakamani, wakageukia kwenye nguvu za giza. Kwa ajili ya kutekeleza mpango huo waliteuliwa wajumbe wanne, wakiwachangia nauli na masurufu mengine, ili waende Muhoro kwa Mganga wa Kienyeji, ambaye alisifika sana kwa wakati ule kwa mambo ya falak (Lamri). Wajumbe walimueleza Mganga makusudio ya safari yao, na nia yao ya kwenda kwa Mganga huyo.

Wakamueleza yaliyojiri huko Nyipara, baina yao na Waahmadiyya, na bila kuuma maneno walitaka Mganga huyo kwa karama zake, awaangamize Wahmadiyya wote. Cha ajabu ni kwamba Mganga aliwaonya vikali sana wale wajumbe na kuwaambia kwamba, Waahmadiyya wanaye Malaika mmoja mkali sana, anaye walinda kwa hiyo nyinyi hamuwawezi, na wala msiwatendee vibaya, vinginevyo mtalaanika. Mzee Uwesu Sozingwa anasimulia kwamba wale wajumbe hawakurudi tena Nyipara. Michango waliochangiwa kwa ajili ya safari, wakatokomea nayo Dar es salaam. Na hawakurudi mpaka mauti yamewakuta wakiwa Dar es Salaam.

InshaAllah tutaendelea na Historia inayohusu Jamaati nyingine katika Mkoa wa Pwani katika matoleo mengine yajayo.

Muhajirina wa Kwanza Tanzania



Na

Fadhili

Mshamu

Katika harakati za kuandika historia ya Ahmadiyya Tanzania nilivutiwa na kusisimka kutokana na maelezo niliyopewa na bwana Fadhili Mshamu ambaye nimefahamiana naye toka miaka ya sitini. Nilimuomba atuandikie sehemu hiyo muhimu ya historia.
Nashukuru kwa kuitikia wito na matokeo yake ni hii makala ya kusisimua 'Muhajirina wa Kwanza Tanzania'. Tunalo la kujifunza kutoka kwa Fadhili Mshamu na ni matumaini yetu wenye mambo ya kusisimua hawatasita kutoa wino kalamu zao ili kwa pamoja kushirikiana katika kuhifadhi historia yetu.
- Mhariri.

Ninapenda kueleza historia ya wazazi wangu walivyojiunga na Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya mwaka 1952 wakati huo nikiwa na umri wa miaka 13. Baba yangu aliitwa Abdallah Mshamu Dungurusi na mama yangu ni Somoe Abdallah Omari Umande. Wao waliishi kijiji cha Mtandi Wilaya ya Kilwa Kusini Mkoa wa Lindi. Pia napenda kuweka wazi kwamba katika kujiunga na Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya hakuwa baba na mama pekee bali walikuepo watatu ambao walikuwa ndugu kabisa na marafaiki hasa. Bila shaka mtakuwa na hamu kutaka kuwajua akina nani hao wawili? Mmoja anaitwa Sheikh Issa Haruni Kurunguja na mkewe Fatuma binti Kamtande na mwingine bwana Mohammed Suleiman Mkoka na mkewe binti Omari Umande. Wote kwa ujumla walijiunga na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mwaka 1952 chini ya uongozi wa Khalifa mtukufu wa pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad r.a.
Marafiki hawa wapendwa wakiwa wakipendana sana na walikuwa Ahaldhikri, walikuwa chama chao Qadiriyya. Hapo kijijini kulikuwa vyama vya dhikiri ni viwili. Qadiriyya na Shadhiriyya. Basi kulikuwa mashindano makubwa kati ya vyama hivi viwili vya dhikri kama tuonavyo timu za mpira. Kwa hakika Sheikh Issa Haruni Kurunguja alikuwa msomi mzuri wa Quran Tukufu na alikubalika sana katika vijiji jirani pia alipewa msikiti wa Mtandi asalishe na kutoa mawaidha. Lakini hayo yote yaliharibika baada ya kujiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Bila shaka mtapenda kujua waliupata vipi ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa^{as}. Kwa hakika Jumuiya hii hata uwe katika Kijiji kisichojulikana kidogo sana na dhaifu lakini ujumbe lazima utakufikia tu. Ujumbe umefika kwa Khalifa Mtukufu wa pili kumtuma Sheikh Fadhlillah kuja mkoa wa Lindi. Ingawa alipata taabu sana lakini alifanikisha kupata wanajumuiya kusini. Wenzetu wa Lindi na Mtama Jangwani walianza kumpokea Masihi Aliyeahidiwa. Kabla ya Mtandi, napenda kueleza kwamba ukitoka Mtandi kuna Kijiji kidogo sana kwa wakati ule wa 1952 kiitwacho



Abdallah Mshamu Dungurusi

Kilanjelanje. Alikuwepo Sheikh Issa Lichila. Yeye alianza kumpokea Masihi. Bwana Mohammedi Suleimani MKoka yeye alikuwa mfanya biashara wa ushanga, hereni, pete, n.k. Akienda Lindi mara kwa mara baada ya kumaliza biashara zake alipata kuonana na Sheikh Fadhlillah. Watu hawa wawili ndiyo waliowasha taa hii Mtandi. Baada ya kupokea ujumbe huu kijuujuu ilimbidi Sheikh Issa Haruni Kurunguja aitwe Sheikh Issa Lichila aje Mtandi ili aeleze mada kuu mbili; Kuendelea kwa Utume na Kifo cha Nabii Issa Mwana wa Mariam. Kwa hakika alifika kuelezea mada hizo kuu mbili. Mjadala ulikuwa na watu wengi lakini wengi hawakuelewa lakini pale walioelewa ni watatu tu; Sheikh Issa Harun Kurunguja, Bwana Mohamed Selemani Mkoka na Abdallah Mshamu Dungurusi na wakachukua Ba'iat siku hiyo hiyo. Kuanzia siku hiyo amani ikatoweka ikawa uhasama mkubwa sana wakisema Bwana Issa Lichira kaharibu Mtandi kauleta Ukadiani na kuwateka ndugu zetu hawa watatu. Wakasema wale wapinzani kwamba tutafanya kila njia ili kuwarudisha katika Uislamu sahihi kama hawataki kurudi tutawafukuza wasiharibu Mtandi. Kusema kweli kulikuwa na vuguvugu kubwa sana mpaka vijiji jirani vya ukanda wa Pwani vikapata habari mara moja tukianza na Kisuwele, Rushungi, Mabanda Mbache, Limalyao, Kisongo, Ruwango, Pande, Mtandura, Masoko hadi Kivinje kwamba Mtandi Umeingia Ukadiani na kuna Mtume mwingine baada ya Mtume Muhammad^{saw}. Kwa hakika baba zetu waliteswa sana nasi Watoto tulikuwa tunasemwa sana na watoto wenzetu tukiambiwa tumepigwa mihuri matakoni na baba zenu na mama zenu na kutuambia mna njaa sana kukubali kununuliwa na Wahindi hawa. Wakati ule ilikuwa ni aibu sana kuitwa Kadiani na kuambiwa Mtume wao Mirzai ni ponjoro. Baba zetu wakitoa salam hakuna wa kuitikia, hata maji ya kunywa kikombe tunachotumia sisi si ruhusa kutumia Waislam wengine. Kweli sisi tulionekana makafiri kwani tumeritadi, tumetoka katika Uislam wa Mtume Muhammad^{saw}. kwa kujiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Kutimiza ahadi yao ya mateso ilikuwa shughuli zote za Kiserikali wao ndio wa kwanza kuambiwa wasipokwenda wanashitakiwa na kupigwa faini. Baba zetu waliteswa sana. Wakaona bado wanang'ang'ania Ahmadiyya wakasema tukutane wazazi tuliowaozesha watoto zetu tuwashitaki ili tuwachukue tusiwaachie makafiri. Kweli walifanya hivyo. Sheikh Issa Haruni Kurunguja, Mzee Mohamed Sulemani Mkoka na Mzee Abdallah Mshamu Dungurusi walishtakiwa na wazazi wa wake zao. Kesi hiyo ilifunguliwa Mahakama ya Mwanzo Mtandi na Hakimu Jumbe Amri Mmanja. Mashitaka yalikuwa hivi:- Kila mzazi asimame na mtoto wake na mkwe wake na kutoa maelezo mbele ya Mahakama sababu ya mashitaka na kila ammoja atajibu shitaka lake. Ingawa shitaka lilikuwa moja tu, ambalo ni hili; "Nimemshitaki Bwana Abdallah Msham nilimwozesha mwanangu kwa sharia ya dini ya Kiislam inayoongozwa na Mtume Muhammad^{saw} lakini mkwe wangu huyo katoka katika Uislam amekuwa Kadiani ana Mtume mwingine Mirzai, kwa hyo hafai kukaa na mwanangu atampoteza". Shitaka lilikuwa moja tu lakini kilamshitakiwa atajibu kwa wakati wake. Atakapoitwa na kusimama baba, mume na mke wake. Alianza baba. Yaani Mzee Abdallah Msham kujibu shitaka hilo. Alisema "ninamshukuru sana mzazi wangu kwa aliyoyasema kwamba ameniozesha mwanawe kwa sharia ya Islam iliyoletwa na Mtukufu Mtume Muhammad^{saw}. na mpaka sasa ninao Uislam ule ule anaoufahamu yeye. Lakini baba haelewi Mtukufu Mtume Muhammad^{saw}. aliahidi nini mbele ya Waislam? Alisema nikiondoka mimi atakuja Masihi wangu atakayefikisha Uislam pembe zote za dunia. Sasa sisi tunazingatia agizo hilo. Lakini sishangai hilo ni jambo la kawaida Mitume wote wanaotumwa na Allah hawapokelewi kwa sherehe lazima wakataliwe. Hata Mtukufu Mtume Muhammad^{saw}. walimkataa na kumsema Muongo (Mungu Apishe mbali). Kawaida. Basi mimi ni Muislam safi nimefuata agizo la Mtume wetu Muhammad^{saw}". Hapo aliishia. Akaitwa mkewe kwa jina akaulizwa; baba yako umesikia alivyosema, je wewe unasemaje? Akasema mimi sioni kosa analolifanya mum wangu hata moja, kwani kwa baba nilikuwa sijui kutawadha, kwa baba sikujua kusali, kwa baba sikujua umuhimu wa kufunga saumu. Mambo haya yote nimeyajua kwa mume wangu. Kwa baba

Inaendelea uk. 5

Muhajirina wa Kwanza Tanzania

Kutoka uk. 4

nilijua kwenda ngomani, hitima, tatu, matanga, n.k. Nilifikiria ni dini kaagiza Mtukufu Mtume Muhammad*saw*. Maneno ya baba siyaafiki kwamba mume wangu kapotea. Mimi ninalolijua anafuata muongozo wa Mtukufu Mtume Muhammad*saw*. kwa hakika zilitoka radhi hapo tangu leo si mwanangu tena mpaka siku ya kiyama. Umma uliohudhuria pale ukamsakama sana mama. Akaja wa pili Mzee Mohamedi Sulemani Mkoka. Huyu mke aliyeoa mama shangazi yake kwa hiyo alisimamia kaka yake. Ni yule baba yake mama yaani Abdallah Omari Umande. Kwa kuwa alianza kwa mtoto wake, na majibu aliyapta hakuwa na nguvu sana upande wa dada yake. Mzee Mohamedi Sulemani Mkoka alisomewa shitaka lake la kutoka Uislam wa kweli na kuingia katika dini ya Mtume mpya Mirzai Kadiani. Yeye alijibu shitaka hilo kama ifuatavyo; “mimi nimemuoa dada yako kwa sharia ya Allah aliyepewa Mtukufu Mtume Muhammad*saw* na mpaka sasa nafuata sharia hiyo hiyo. Sijabadilisha ila watu hawafati Quran Tukufu wala Hadithi na Sunna. Kwani hata Mtukufu Mtume Muhammad*saw* alishasema katika Hadithi kutoka kitabu Bukhari hakutabaki Uislam ila jina, hakutabaki Quran ila maandishi tu, na misikiti yao itajengwa mikubwa lakini haina muongozo. Masheikh na Walimu watakuwa wabaya chini ya mbingu. Mufahamu wakati huu Masheikh wachochezi wakubwa hawataki kufuata maandishi ya Quran na Hadithi wala Sunna. Namalizia hakuna dini mpya wala Mtume mpya, yote yapo ndani ya Quran Tukufu na vitabu vya Hadithi. Watu walijaa sana siku ile. Makadiani wananyang’anywa wanawake. Kulizwa mke akajibu yote mashitaka nimeyasikia aliyokuja nayo kaka Mahakamani hapa. Mimi ninamuuliza swali; wakati ninakwenda ngomani kucheza. Hakunikataza nakwenda ziarani kuchanganyika na wanaume na wanawake wala sikukatazwa. Mume wangu ananikataza mambo haya aaonekana kadiani nikamchukue dada yangu. Majibu hakujibiwa mke wa Mzee Mkoka alimjibu kaka yake hivi wewe kaka mimi nduguyo hatuzikwi kaburi moja kila mtu atalipwa alichokichuma. Simwachi mume wangu kufuata fitina zenu za Masheikh wenu. Watu wawili wakamaliza hoja zao akabaki Sheikh Isa Haruni naye akaitwa kizimbani na mkewe. Sheikh Issa Harun Kurunguja hakuwa na taabu sana kujibu mashitaka. Haya si mageni kwangu, hata Mitume walishitakiwa. Mtume Mussa alitaabishwa sana na Firauni; Issa wa jina wangu alishitakiwa na Pilato; Nuhu alipata taabu sana akasaidiwa na Allah; Lut kapata taabu sana na watu wake, Allah Akasaidia wakaangamizwa watu wake; Mtukufu Mtue Muhammad*saw* alipata taabu sana na ndugu zake mpaka akahama kwa amri ya Allah kuhamia Madina. Je! Mimi na Mitume hawa nani mbora? Naona haw ani bora sana. Hawa nimewataja wachache sana Mitume waliopatishwa taabu. Mimi sioni ajabu kufikishwa hapa lakini mumipata taabu sana mungalikuja tu nyumbani kuniambia tunamtaka mtoto wetu wewe Kadiani mimi ningalikuambieni mchukueni mchukueni. Mimi sina pingamizi mchukueni. Sheikh Issa kamaliza Bwana Omari Mussa Masapanga akamchukua kwenda naye nyumbani lakini ilikuwa kasheshe huko nyumbani. Baada ya siku tatu akarudi kwa mume wake wakaendelea na Maisha. Baada ya kesi hiyo kukazidi mateso sana. Kuanzia 1952 hadi 1954 wazee hawa walikaa pamoja wakajadili kuhama kwenda Lindi. Akatumwa Mzee Mohamed Sulemani Mkoka kwenda Lindi kuonana na Sheikh Fadhlillah, Sheikh Ahmad Mataka na Mzee Karuma Issa. Alipokwenda kuonana na Masheikh hawa na kuwaeleza habari hizi akaambiwa muje huku. Aliporudi Mzee Mkoka kuleta habari ya kukubaliwa kuhamia Lindi wakajitayaraisha kuhamia Lindi 1954. Tulipokelewa vizuri sana na wenyeji wetu. Mzee Abdallah Mshamu na Mzee Mohamed S. Mkoka walifika kwa Sheikh Ahmad Mataka. Sheikh Issa Haruni Kurunguja alifikia kwa Mzee Issa Karuma. Baada ya kukaa miezi mitatu…

Itaendelea toleo lijalo

Tumia Chombo Hiki Usalimike



Na Khamis Wamwera

Kwa elimu ambayo Subhana Wata’ala Amempa mwanadamu, kwa hakika imekuwa ni kazi na Hazina kubwa ya maendeleo duniani. Watu wameitumia kwa matumizi mbalimbali. Katika elimu hiyo, wapo watu waliofika mwezini na kuweka vitu vyao. Bali kubwa zaidi ni lile la kutambuwa Allah yupo hai na Yeye Ndiye Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo humo. katika fadhila hii kubwa ya elimu, yule aliyeipata na pia akawa na amali njema, huyo anafanana na ule mti wenye majani mapana ambapo wasafiri hunufaika kwa kivuliche. Hili halina shaka , kwa sababu ya elimu, watu wameweza kutengeneza vyombo aina kwa aina kurakhisisha kadhia ya usafiri. Kwa kutumia mali ghafi ẏa ardhi, wenye elimu wameweza kuunda baiskeli, magari, magari moshi, merikebu, meli na madege na vyombo kadhaa vya angani. Shabaha na malengo ni kuufanya usafiri uwe mwepesi kwa ajili ya watu na mizigo yao na kwa mafao mengine.

Naam, pamwe na juhudi na maarifa haya yote ya watu, bado vyombo hivyo na vingine, vina dosari na upungufu mwingi tu. Magari moshi huacha reli na magari hupinduka. Meli na Merikebu huzama. Madege na vyombo vinapukutika,vitu vilivyomo humo vyote husagwasagwa kama unga na watu waliokuwemo humo huangamia wakawa tikitiki.

Hapa hivi leo, mimi napenda kukuonesha wewe msomaji wangu mpendwa chombo kimoja madhubuti sana. Kwacho wenye akili na busara hukitumia katika safari zao za masafa marefu. Hicho kipo imara na kimeundwa kwa vifaa visivyoguswa na kumeng’enywa na kutu wala kupata udhaifu wowote. Hicho kinapambana na kila aina ya sulubu na misukosuko kamwe hakipinduki kwenye ardhi, hakizami baharini na wala hakianguki kutoka juu angani. Wakati wote kipo salama usalimini. Abiria wake daima huwa hawana khofu wala wasiwasi.

Kwa wewe ambaye hujakiona chombo hiki na pengine umekiona waila hujakwea, basi hapa sasa kwa ufupi nitakujulisha.

Kwa kweli chombo hiki kimeundwa kwa umahiri mkubwa na ustadi unaokubalika. Ni chombo chenye injini isiyovuja na wala hakitoi mvuke na moshi. Injini yake yenyewe ni SWALA. Magurudumu yake hayahitaji kubadilishwa kwa sababu ya kusagika nako ni KUHIJI MAKKA. Usukani wa chombo hiki mna viti vya dhahabu vya kukalia, nawe uwe mchafu namna gani utapewa kwa kutowa ZAKKA. Ukitaka kufahamu taa ya chombo hiki ni nini, basi ni SWAUMU.

Ni chombo adimu sana, lakini watu wengi hawakitumii. Sijui kama hawajakiona au ni kwa ajili ya kiburi chao tu! chombo hiki ni kikubwa na kinachukuwa abiria wengi khususa wale wapenda salama. Hiki ni chombo kinachosafirisha watu kutoka hapa duniani na kuwafikisha peponi. Kituo chake kipo msikitini na mkata tiketi wake ni malaika. Mwongozi wa chombo hiki ni Amal Njema na ufunguo wa chombo ni kutowa shahada mbili. Nilisahau, nauli ya kutoka hapa hadi peponi ni kutamka kwa dhati na uthabiti wa moyo kwamba Hayupo anayestahili kuabudiwa kwa haki ila Allah na kuwa Muhammad*saw* ni Mjumbe Wake.

Basi nakuomba ndugu yangu mpendwa ufanye haraka. Nenda pale msikitini kakate tiketi yako maana chombo kinaweza kuinua safari wakati wowote. Tiketi yenyewe ni udhu na abiria wenyewe wa chombo hiki ni wale wote waliowanyenyekevu, Wacha Mungu na watawa. Nakuombea safari njema. Wabillah Taufiq.

Bustani ya Washairi

CHUNGU

Mola ilahi Rabuka, Nashukuru sana
Shukurani za hakika, za kwangu miye kijana
Chungu nimeshakiwekan ndani kimetulizana
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Hata mkinishawishi, chungu siwezi kitoa
Ladha yake na mapishi, ndo inayonikoa
Wala sio kwa utashi, kwamba nilizoa zoa
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Chungu changu ni kizuri, Mola Kanijaalia
Kanitunuku Ghafuri, kizuri hakina doa
Vileja pia kachori, ndani ninajipikia
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Maanjumati jipikia, mengi ya kitaalamu
Ladha kinavyonipatia, tena imezidi tamu
Waja mimi natongoa, chakula chake adhimu
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Pindi ninapopikia, ndo kinanipagawisha
Pale ninapoepua, chakula nikiivisha
Hapo ndipo nakodoa, chungu bado chachemsha
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Na tena kimejaaliwa, hasa kwa umbile lake
Mwenzenu mi nachachawa, hakuna mithili yake
Ukweli huwa najuwa, kwamba wapi nikishike
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Nawashangaa wenzangu, pale mnanilaumu
Haya maamuzi yangu, nataka munifahamu
Sasa kimo ndani kwangu, kwangu ndio mahamumu
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Wala mimi sitokuwa, kama wale wendawazimu
Nyungu wakazinunua, kisha wenda kwa mizimu
Mwisho wakavipasua, eti tiba ya kitaalamu
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Jama chungu hururi, ndani sikiachi peke
Nitakilinda kwa uturi, ili wasije kiteka
Nami ninakisitiri, mikononi kisitoke
Sikiachi chungu changu, hata mkinishawishi

Mwisho natuma salamu, wangu Lusanga wapenzi
Siku moja ikitimu, chungu nakileta enzi
Na nyinyi mkifahamu, sio mimi tu kipenzi
Sikiachi chungu changu, nimekipenda mwenyewe

Rajabu Abbasi Mkieti,
Al Wattan Mlezi, Muheza, Tanga

Mola Kisitiri chungu, kizidi kuimarika
Kila tone la uchungu, mwisho liweze kauka
Usafishe na ukungu, jua lipate
Usiache chungu chako, masikio weka pamba

Chungu hutoa machungu, roho ikatulizana
Hutanda kama mchungu, kivuli kupatikana
Hino ukweli wa tangu, si wa leo au jana
Usiache chungu chako, masikio weka pamba

Mhariri

NDOA

1.Nalikunjuabusati,karibuniwngwana,
Tenakwamoyowadhati,siper{dikubanabana,
Tungalikowasaliti,baadhiyetunaona,
UkhalifaTwaukana,ndoanjeyajamaati.

2.Mazoeasiocheti,wajifanyahujaona,
Ewemwanajamaati,maradhihautapona,
Nazaidihatihati,nikuangamizawana,
·Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

3. Kiroho siha hupati, shirki utaivuna,
Utawekwamtukati, nandevuakizikuna,
Bidaakilawakati, nduguujanjahauna,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

4.Naombababababahati,ulemchangowajana,
Ulewakicheniparti,naulewangomabwana,
Khitimayavingunguti,unipeharakasana,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

5.Ukondaniyakabati,huwezitenakunena,
·Hutoihatasauti,umebakikunong'ona,
Pesahizokwenyekoti,aakupendabi.zuwena,
Ukhalifatwaukana,nd,oanjeyajamaati.

6.Mashartiyabayati,tuyazingatiesana,
NiwaMungumkakati,..Sisikuhurumiana,
Wapowengimabanati,nawazurikilakona,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

7.Hinokwetunishuruti,kwamabibinamabwana,
Atfalinasirati,kwakhuddamnalajna,
Lazimachinituketi,tuyasemekwamapana,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

8.Ansarnakamati,zinginezondioshina,
Tuzisomsninyakati,Ukwelikuambiana.,
Chenyemotokizingiti,yaniniwaking'ang'ana,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

9.Sasanaifunganati,tuombekwamaulana,
Njiaiwehasanati,zetukookuungana,
Nashukalasamawati,litufunikevijana,
Ukhalifatwaukana,ndoanjeyajamaati.

Mwl. Najat Fakim Said Nangolo
The Big Boss - " Pawaga- Magozi- Iringa"

MAMA YANGU WA THAMANI

Bismillahi Khaliqi, nchi kavu na majini
Kunipa mimi Wahaqi, wa thamani maishani
Namboraye Razaqi, Msaada Abadani
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Mama yangu wa thamani, namlinda simtoi
Kama vile yangu mboni, namuweka kama tai
Mengine simtamani, wala mwengine sijui
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Heshma yake tukufu, naitoa kwa yakini
Hata ukiwa dhaifu, mama ni mama jamani
Hata ukiwa mchafu, hakutupi abadani
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Amenibeba tumboni, miezi tisa shidani
Hata awe na huzuni, anikani abadani
Sitoacha mthamini, mpaka naingia chini
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Siku zilipobaini, kunitoa duniani
Chozi laanguka chini, huku yeye aamini
Ajui afanye nini, kulinda kilicho tumboni
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Mzazi wangu jamani, mwana anipenda sana
Ndivyo hata kwenye dini, humtukuza wake mwana
Hata awe taabani, mama mkarimu sana
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Mama shinda nyumbani, mimi kunihudumia
Hata nianguke chini, mama hunikimbilia
Miumwe hata kuchani, yeye hilo hulijua
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Abadani hanichoki, hilo ninalieleza
Na mwengine simtaki, huyu ananipendeza
Hata mkinishitaki, sitaki kumpoteza
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Nikiondoka nyumbani, kwa sheriaze za dini
Mi kuwekwa hatarini, taka kwake mikononi
Ye hulia kwa huzuni, furaha iso kifani
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Tena watahadharisheni, wote wenye kumkana
Pengine wakamchosha, mama kumfanya mwana
Mola Amempandisha, na daraja kubwa sana
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Hakika siwezi sema, uzuri umekithiri
Mama kwa mwana ni mwema, tena ninayo fahari
Na wala hana karama, tuseme ni mashuhuri
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Tena si wa miujiza, na wala si malaika
Mama ninampongeza, kwa yale yake mashaka
Baya likijitokeza, hulitatua haraka
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Hana kinyongo moyoni, tena anatembeleza
Furaha iso kifani, moyoni ameeneza
Tena nawaambieni, msije kumpoteza
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Hakika mama yakini, jinale nalitukuza
Hata angekuwa jini, mchawi anaongoza
Ila mama ana dini, hilo ninampongeza
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Wallahi Mola manani, Ameagiza jamani
Wabil walidaini, yaliyo ya ihsani
Na tusipowathamini, basi tupo hasarani
Mama yangu wa thamani, Akhera na duniani

Afsal Said Mpanga
Magomeni Kagera, Dar es salaam

NDOA

Salamu zangu jamia, ndugu zangu Islamia
Wajibu kuitikia, ni sunna kusalimia
Kaagiza Ashimia, nusu ya dini sawia
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Katuumba mbeya mbili, ya kike na kiume
Na tufe si kunawili, na mazuri tuyachume
Tutulize si akili, na elimu tuzisome
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Na yale yalo muhali, kwa mwanau kuoa
Kuoa wake wawili, watatu na nne pia
Na kuwapa ya halali, haki wanojitakia
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Na mwanamke sikia, mume ndio ngao yako
Na usipozingatia, hasara ni juu yako
Haraka we itikia, akikwita mume wako
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Mume karudi kazini, ataka ye kujaliwa
Nawe simu mkononi, vya humo vyakuzuzua
Hujali ataka nini, nawe hofu hujagewa
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Kwenye maisha ya ndoa, tafuta anokufaa
Na mwenye dini sawia, uzuri wake murua
Nasaha yake saidia, mali alojichumia
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Mchunguze wako mwenza, kwa utulivu na wema
Usikurupuke kwanza, kwa mabay kumsema
Ibada bora kufanza, ujaliwe alo mwema
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Ila jema nawambia, talaka mbaya hakika
Shetani hufurahia, na mbingu kutikisika
Huzuni yanyemelea, kwa wale wanaohusika
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Machache nilowambia, ni vyema kutyachukua
Japo sikupambanua, kwa umri batwia
Na kalamu naitua, usije tu puuzia
Ndoa sio lelemama, yapasa kuzingatia

Nuni Adam Mpanga
Magomeni Kagera, Dar es salaam

HAE! MSIBA MZITO

Hae! Msiba mzito
Wachoma mithili moto
Na pembeni kuna joto
Roho hazijatulia

Umelileta fukuto
Kwa wazee na watoto
Msagiko wa kokoto
Ni wadogo tumekua

Mwinshehe bini Juma
Sisi katuacha nyuma
Amerudi kwa Karima
Fungulake kupokea

Shajarali ya neema
Ya matunda ya neema
Tena yaliyo imama
Ni sururi kujilia

Ni kilio na huzuni
Wanajamati nchini
Kuondoka muhisani
Kwa Mola amerejea

Sote tumo makiwani
Kile kifo cha thamani
Kimetoka duniani
Uchungu katuachia

Kazi zote za Jamaati
Alizifanya kwa dhati
Na tena kila wakati
Labeka kuitikia

Ya Ilahi Mola Izati
Walio wote umati
Peponi apate kiti
Tunakuomba Jalia

Kwenye Jalsa Salana
Ilikuwa ni bayana
Utamdhani kijana
Kitako hakutulia

Kazi za kila namna
Hakuna aliyekana
Kazifanya kwa kufana
Pasi jambo kufungua

Ni Wewe Maliki Nasi
Tena Ilahi Nasi
Mpe yalo na ukwasi
Yale Uliyoridhia

Kaditamati na sisi
Utupatie nemsi
Tuyaepuke maasi
Tuishike hino njia

Mahmood Hamsin Mubiru - Wa Mamba

Kunoa

Palikuwa na kundi la wanaume – kijana mbichi, mwenye nguvu (shababi) na idadi kubwa ya wazee, wakifanya kazi ya kukata miti msituni.



Huyu kijana ni mchapa kazi sana. Alikuwa akiendelea kufanya kazi hata mapumziko na alilalamika kwamba wale wazee walikuwa wakipoteza muda, wakipumzika mara kadhaa kwa siku wakinywa na kupiga soga.

Siku ya kwanza, kijana yule alikata miti kumi na tano (15). "Hongera", bosi alimwambia,"endeleanakaziyako!". Akiwa motisha kutokana na maneno ya bosi wake, alijaribu kw bidii sana kesho yake, lakini alikata miti kumi (10) tu. Siku ya tatu alijaribu kwa bidii zaidi, lakini aliwez kukata miti saba (7) tu. Siku hadi siku alikata miti kidogo na kidogo zaidi.



Kadri muda ulivyokwenda, kijana huyu aliona kwamba licha ya kufanya kazi hata bila ya kituo na kupumzika kwa akali, wale wazee wanakata kiasi sawa cha miti kama alivyokata yeye na wakati mwingine kumzidi. Ilikuwa kana kwamba wale wazee walifanya kazi aliamua kwa bahati mabovu nguvu alifikiria. bila mapumziko kama yeye. Hivyo kuongeza bidii siku iliyofuatia, mbaya matokeo yakawa zaidi. "Itakuwa naishiwa zangu". Kijana mkata miti

Siku moja, wakata kinywaji wakati kijana alikataa na akasema mmoja kati ya wale wazee miti alimualika kwa ajili ya wa mapumziko yao. Yule hana muda wa kuchezea! Basi mzee akatabasamu akamwambia kuwa ni upotezaji wa nguvu na juhudi bure kuendelea kukata miti bila ya kunoa shoka lake. Utakata tamaa au kuchoka mapema kwa kutumia nguvu nyingi sana.

Ghafla Yule kijana akagundua kwamba hasa nyakati za mapumziko wakati wale wazee wanapiga soga, walikuwa pia wakinoa mashoka yao muda huo huo! Ndio maana waliweza kukata miti mingi kumshinda yeye na kwa muda mchache! Mzee akamwambia Yule kijana kwamba tunachohitaji ni ufanisi kwa kutumia ujuzi na maarifa yetu kwa akili. Hapo tu ndipo tunaweza kuwa na muda zaidi kufanya na mambo mengine.

La sivyo mara zote utabakia kusema.. Sina Muda!

FUNZO: kwa kuweka kituo katika kazi, itakufanya kusikia murua, kufikiria vizuri na kufanya vyema baada ya mapumziko! Lakini kwa kuweka kituo, si kuacha kazi bali kupumzika na kuitafakari upya mbinu na kuiendea kwa mtazamo mwingine. Pia, wengi wetu hatuongezi maarifa na stadi zetu. Tunafikiria kwamba tulichojifunza kinatosha sana. Lakini kizuri si kizuri kinapotarajiwa bora. Kuyanoa maarifa yetu mara kwa mara ndio ufunguo wa mafanikio.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

AHMADIYYA	GAZETI	ISTIKHARA	NCHI	SHARI
AMANI	HINDU	LUGHA	NGAMIA	UHURU
BIDAA	INSHA	MAMLUKI	NJIWA	YAUM
BUDHA	ISLAM	MUUJIZA	SABATO	

U	W	J	T	W	G	L	U	G	H	A	X	M
H	J	I	C	I	H	K	R	R	A	J	I	U
U	M	S	K	M	N	M	L	Y	Q	N	S	U
R	A	L	G	T	U	S	Y	R	I	J	T	J
U	M	A	Y	A	S	I	H	R	G	I	I	I
K	L	M	Y	Y	D	A	A	A	A	W	K	Z
G	U	L	G	A	U	H	B	I	Z	A	H	A
H	K	T	M	N	S	S	N	A	E	X	A	N
N	I	H	K	Q	G	A	U	L	T	D	R	Z
P	A	N	V	T	M	K	Z	F	I	O	A	M
F	H	L	D	A	X	N	Z	B	U	G	D	B
C	J	N	M	U	L	N	G	A	M	I	A	R
P	T	N	C	H	I	Q	T	B	U	D	H	A

CHEMSHA BONGO

Je unaweza kuoanisha wanyama na sura za Qur'an Tukufu walimotajiwa? Hebu onyesha!

Ngamia	Sura Al A'raaf
Farasi	Sura Al Qalam
Kondoo	Sura Al Ankabut
Kunguru	Sura Al Fiil
Ng'ombe	Sura Al 'Aadiyaat
Nyuki	Sura As Saaffaat
Nyani	Sura Luqmaan
Tembo	Sura An Nahl
Nyangumi	Sura An Naml
Punda	Sura Al Maaida
Nguruwe	Sura Al Baqara
Buibui	Sura An'aam
Mbwa	
Nyumbu	
Mbuzi	



Majibu ya Chemsha Bongo la Toleo la Februari: *Hongereni mliopatia yote*

1. MISIKITI	5. ATFAL	9. IAAAE	13. KHUDDAM	16. HIJA	19. JAMAA	23. SANDA
2. SALA	6. TABLIGH	10. ASILI	14. SUNNA	17. AMINI	20. AMANA	
3. AMANI	7. AZALI	11. TANZIM	14. SHURA	18. DINI	21. AHAD	
4. ISMAIL	8. ILIKI	12. ASIDI	15. AKILI	19 JIHADI	22. IHRAM	

Mkutano wa Amani Wafanyika Kanisani







Na **Mwandishi Wetu**

Kwa fadhila za Allah, Jumuiya ya Waislam ya Ahmadiyya Tanzania imeandika historia mpya katika nchi yetu kwa kufanikiwa kufanya mkutano wa amani uliofanyika ndani ya Kanisa la Wasabato katika viunga vya Temeke jijini Dar Es Salaam.

Akiwa mgeni rasmi wa Mkutano wa huo ulioandaliwa na kanisa hilo, Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry alifika kanisani hapo saa tano na nusu asubuhi na kupokewa na wenyeji wakiwemo Wachungaji na Maaskofu wakiongozwa na Askofu Mkuu wa jimbo la Kusini Mashariki Ndugu Steven Ngusa na Mchungaji Dominick Pius Mapima ambaye ni mratibu wa mahusiano ya kidini kanisa hilo kwa jimbo la kusini Mashariki. Pamoja na hao walikuwa wazee wa kanisa na wahudumu mbalimbali na waumini wa kawaida kanisa hilo.

Baada ya kuweka sahihi kitabu cha wageni na kupata utambulisho wa muundo wa kiuongozi wa Kanisa, Amir akiongozwa na Askofu Ngusa alikaribishwa kufungua mkutano huo kwa hotuba ambayo aliwapongeza viongozi wa kanisa hilo kwa kuratibu mkutano huo mzuri na wenye manufaa kwa binadamu wa dini zote mbili. Amir sahib aliweka wazi kuwa mikutano ya amani ni jambo ambalo Jumuiya hii inalipenda na alipopata fursa ya kuja alifurahi sana na hii inaondoa chuki miongoni mwa waumini wetu na pia alitumia fursa hiyo kuwakaribisha waumini wote wa kanisa la wasabato kuhudhuria mkutano wa mwaka wa Jumuiya utakaofanyika mwezi septemba. Amir aliongoza maombi ya kimya na hivyo kufungua rasmi mkutano huo ambao pia Sheikh Asif Mahmood Bhati na Sheikh Abdulrahman Mohammed Ame walitoa mada kwa upande wa Ahmadiyya, watoa mada kwa upande wa Wasabato walikuwa ni Mchungaji Dominick Mapima na…….na kufuatia kipindi cha maswali na majibu. Amir sahib alihojiwa na vyombo vya habari vya TBC, VoA na vingine vingi ikiwemo gazeti hili la Mapenzi Ya Mungu.

Mkutano huu ulifungwa rasmi saa 12 jioni na Askofu Mkuu wa jimbo la Kusini Mashariki Mchungaji Steven Ngusa kwa maombi. Wasabato na Waahmadiyya wote kwa pamoja walikubaliana kuenzi amani kwa dini zetu chanzo kimoja ambaye ndiye muumba wote na hivyo kuahidi kuendelea kuwasiliana na kufanya mikutano kama hii zaidi ikiwa ni pamoja na kutembeleana katika kuimarisha udugu na umoja wetu huo.



ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA
Dhihirisho la Pili

Basi, enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndiyo sunna ya Allah tangu kale ya kwamba Mwenyezi Mungu Huonyesha kudra mbili ili kuzikanyagilia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aziache sunna yake ya zamani.

Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifazaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu kwa sababu hiyo itadumu, nayo itaendelea bila kukoma mpaka Kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakini niondokapo, hapo Mungu Atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu nanyi milele kama Mungu Alivyoahidi katika Barahini Ahmadiyya. Ahadi hiyo hainihusu mimi bali yawahusuni ninyi, kama Alivyosema kwamba Nitashindisha Jumuiya hii inayokufuata juu ya wengine hadi Kiyama.

Basi hakuna budi mfikiwe na siku ya mimi kuagana nanyi ili baadaye iwadie ile siku iliyo siku ya ahadi ya kudumu. Mungu wetu huyu ndiye Mungu Atimizaye ahadi, Mwaminifu na Mkweli. Atawaonyesheni yote Aliyoahidi. Ijapokuwa hizi ni siku za mwisho za dunia na ndiyo zama za balaa nyingi kushuka, lakini hakuna budi dunia hii ibaki mpaka yote hayo yatimie Aliyoniambia Mungu. Mimi nimedhihirika nikiwa kudra moja kutoka kwa Mungu, nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwapo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili. Hivyo basi, endeleeni kuomba mkiwa pamoja ili kuingoja kudra ya pili ya Mungu. Na yawapasa wanajumuiya wema wa kila nchi wakiwa pamoja kwamba wadumu kuomba ili kudra ya pili ishuke kutoka mbinguni na iwahakikishieni kwamba Mungu wenu ndiye Mungu Mweza hivyo. Fikirini mauti yenu kuwa karibu. Hamjui saa hiyo itawadia lini.

Al Wasiyyat

Je Wajua?
Maombi ya Makhalifa Hukubaliwa Haraka



Mnamo tarehe 26-7-2017 alipatikana Mwana wa Baraka.

Wazazi wa mtoto huyu ambaye ni Bwana Fadhili Pazi na Bi Sakina Digalu walimtoa Waqfu na Khalifa mtukufu alikubali na akatuma jina la mtoto ambalo ni Tariq.

Mama wa mtoto huyu alikuwa akisumbuliwa na masuala ya uzazi zaidi ya miaka 17. Wakati huo wote alikuwa akitumia matibabu mbalimbali bila mafanikio lakini mwaka 2016 alimuandikia barua Khalifa mtukufu na kumuelezea historia ya matatizo yake. Khalifa mtukufu akamjibu barua yake kwamba aendelee na matibabu na kwa msaada wa Allah atapata mtoto. Ni kweli, baada ya muda mchache akashika ujauzito na kupata mtoto wa kiume tarehe 29/07/2017. Alijifungua kwa operesheni. Mama na mtoto walitoka salama, Alhamdulillah Rabbil 'alamiin.

Fanya Biashara, Achana na Riba

Na **Musa Salum Mgeleka**

Enyi mlioamini, msile riba mkizidisha-zidisha; na Mcheni Allah ili mpate kustawi.

Na ogopeni Moto ambao umeandaliwa makafiri.

Na Mtiini Allah na Mtume ili mpate kurehemewa. (3:131-133)

RIBA ni kila deni linalotanguliza kupata faida. Yaani kama mtu anamkopesha mwingine Tshs. 500/= na anamwambia wakati wa kulipa atoe Tshs. 5/= zaidi, au kabla ya kumaliza deni kila mwezi atoe Tshs. 5/=, hii ndiyo riba. Na kama mtu anakwenda kukopa cho chote kwa mapatano ya namna hii pia ni riba. ikumbukwe ya kuwa imekatazwa kutoa riba au kupokea riba. Riba imetumiwa kuwa njia ya biashara, yaani riba imejumuishwa kwenye biashara kiasi hiki tofauti ya biashara na riba ikawa vigumu kuzitenganisha. Na biashara imekuwa wakala wa biashara ya riba. Riba imeingizwa katika mfumo wa kutafuta mitaji ya biashara hasa mitaji inayopatikana kwa njia ya mkopo na kufanya biashara toka mwanzo kufanyika kwa misingi ya riba.

Riba sio tu imekatazwa katika Islamu hata kwenye Kumbukumbu la Taurati 23:19-20 — RIBA ni HARAMU. Licha ya Makatazo yote hayo mwanadamu bado anafanya Biashara ya Riba. Kwanini ni kwa sababu Riba imeonekana kama Biashara zingine. Biashara ni nini ni Kuuza na Kununua Bidhaa na au Huduma kwa mabadilishano ya Fedha. Kusipokuwepo Bidhaa na au Huduma Biashara haiwezi kuitwa biashara. Hata Allah Aliposema Anataka Kufanya Biashara na Wanadamu kwa Kujitolea aliweka kwanza Bidhaa. Anasema HAKIKA ALLAH Amenunua kwa Waaminio NAFSI ZAO na MALI zao ili wapate PEPO 9:111. Hapa Mali na Nafsi zimekuwa Bidhaa na njia ya Mabadilishano yaani (means of exchange) ikawa PEPO. Kwenye Riba Fedha ni Bidhaa na wakati huo huo fedha ndio njia ya Kubadilishana. Hapo kuna upande utakao dhulumiwa kwa Kutoa Riba bila Bidhaa / Huduma na upande utakao faidika na Riba. Upande utakao dhulumiwa na Riba wataongeza gharama za maisha, uzalishaji na uendeshaji na Bidhaa zao kuwa za gharama na bei kubwa wakati wanaofaidika wa Riba hujilimbikizia Mali na Kudhibiti Soko na au Kuwa na Viwanda vikubwa kwa muda mfupi na Kuuza kwa bei nafuu na au ndogo. Na ndivyo matajiri wa duniani wanavyopata utajiri kwa muda mfupi na kuondoa uwezo wa ushindani na Kuongeza umasikini baina ya Jamii kubwa. Na nchi za Africa zimeingia katika Mtego huu wa Kufikiri matatizo yao yanaweza kutatuliwa kwa kukopa kwenye Taasisi za fedha za Matajiri kwa riba. Kila mwaka madeni ya nchi yameendelea kupanda kila mwaka. Kukuwa kwa Madeni kunapunguza uwezo wa nchi kujitawala na kustawi kiuchumi. Mabeberu watafadhili miradi ya maendeleo ili kuendelea kukudhoofisha na kukuangusha kiutawala.

Watu na Mataifa yanayodhulumiwa siku zikija kuamka na kukataa dhuluma hizi, vita kubwa itatokea. Amani inayoendelea kuwepo ni kwa kuwa wanaodhulumiwa wamekaa kimya au kukosa sauti moja. Hali hii huwa haidumu milele, maana Allah Anasema jambo lolote liwe na uzito ndogo kabisa sawa na hardali au likiwa ndani ya mwamba au Mbinguni au ardhini atalidhihirisha tu 31:17

RIBA huondosha HURUMA na Kuwa na MOYO MGUMU na Kujenga UBAHILI na Kujilimbilizia Mali Upande Mmoja. Njia hii Hupunguza Mzunguko wa Fedha kwenye Jamii na Kuondosha Nguvu ya Kununua, huondosha huruma na kuleta uvunjifu wa amani na fujo. Njia hii huongeza Umasikini na ANASA kwa matajiri. Umasikini huwa sababu ya Kudolola kwa Manunuzi ya bidhaa na huduma. Mwisho wa siku pia Tajiri naye huanguka na au kuziingiza nchi zao katika vita ya kiuchumi na hatimaye vita ya Silaha, maana historia inatukumbusha asili ya vita za mababu zetu zilikuwa ni vita zidi ya Mali. Athari za riba hazionekani tu kwa jamii hata kwa mtu mmoja mmoja na familia. Mtu mmoja mmoja na familia hupungukiwa na Mali na kukosa uwezo wa kukidhi mahitaji yao ipasavyo, mahusiano yao hupungua dhana ya udugu huingia mashakani kiasi hiki ili kupunguza gharama na kukidhi haja za msingi, baadhi ya ndugu huzuiwa kufika majumbani na dhana hii familia zinaingia kwenye dhana ya baba, mke na watoto tu wengine sio ndugu. Huku ikiwaacha watu wachache wakiwa matajiri na kumiliki uchumi mkubwa na kufanya matumizi watakavyo kiasi hiki maisha ya anasa kuwa ni jadi yao. Ugumu wa maisha kwa watu masikini na kuwa na imani ndogo huanza kutamani maisha ya matajiri na hatima yake uharifu na uvunjifu wa amani hudhihiri bayana.

Biashara ya Riba ni Maangamio ya Haraiki ya kiuchumi. Kwa kuwa Allah Amekwisha tangaza VITA ya RIBA 2:280. Uchumi umeendelea kupata Mateso kwa sababu ya Riba. Watu binafsi wamefilisika na wanaendelea Kufilisika kwa sababu ya Riba. Taasisi na Serikali zikiangamia, vita zikitokea kwa sababu ya dhana hizi hizi za Kujilimbikizia Mali kwa njia ya Dhuluma ya riba. Biashara zimekuwa na zikipanda na kushuka, kila kukicha Matajiri wanakuwa Masikini na Masikini wanakuwa Matajiri ilimradi uhakika wa maisha haupo. Mataifa yanaanguka na kupotea na kuibuka mengine sababu ya vita iliyojificha ndani yake kuna riba.

Jiepusheni na Biashara ya riba ili kujiepusha na hasira za Allah na yeyote mwenye Akili na Atafakari biashara ya riba kama inamletea faida au la ni mwendawazimu tu atajifurahisha kwa dhana ya faida ya muda mfupi huku akijisahaulisha maangamio makubwa yanayomzunguka. Ili kuepukana na Biashara ya riba ni kufanya njia zote zinazohusikana na Mikopo na Mitaji zimilikiwe kijamii/serikali na zisihusikana na biashara. Kuwepo taasisi za Fedha zisizo na riba katika Jamii na lengo lao lisiwe katika kufanya biashara ya riba ila kutoa huduma ya Mikopo na Mitaji kwa jamii pasipo kuwa na riba. Wakati mwingine taasisi za fedha zikakosa mitaji kwa matajiri kususia kuwekeza fedha zao mahali wasipo pata faida, Islamu inafundisha kuwatoza Zaka kwa mali zao zinazokaa bila kutumika ili sehemu ya Zaka zitumike kuwasaidia Masikini. Kila Mwislamu ajitahidi kujiwekea AKIBA wenyewe ambayo itamfaa kwenye dhiki yeyote ikiwa pamoja na Mitaji. Viundwe Vikundi vya Kuweka na Kukopa ili kujijengea nguvu ya mitaji, sehemu ya Hotuba ya Ijumaa ya Khalifatul Masih V atba ya tarehe 15 June 2007. Shikeni subira ya kila shida zenu ili kujipa muda wa kutafakari na kuzitafutia majibu na sio kila tatizo la kutafutiwa ufumbuzi wa pesa na tafuta kila sababu yeyote sawa na uwezo wako ilimradi ukajiepushe na biashara ya riba kwa sababu tu ya Hofu ya Allah. Allah Atakutenenezea njia bora zaidi.

Waislamu wasifikiri kujitenga kwao katika uchumi wa riba kuwa wata kuwa masikini, kukosa Mitaji, bidhaa na huduma za msingi za maisha yao, hapana ila watambue idadi yao ni kubwa kabisa kusimamisha uchumi wa Kiislamu. Asili ya biashara inahitaji uwepo wa watu angalau kuanzia wawili tu (Mtu wa Kuuza na Mwingine wa Kununua), hii ni kutoka kwenye maana ya biashara. Kila jamii na familia na familia inawezekana kuwa na mfumo wa Kiislamu, ni jambo la kushangaa kukumbatia uchumi ambao unaomchukiza Allah na Waislamu wakiamua kuachana na uchumi wa riba jamii itabadilika tu maana wao ndio wanaohitaji dunia zaidi ya Waislamu. Uchumi bila riba Waislamu watajenga uwezo mkubwa wa kuzalisha, kuendesha shughuli zao kwa gharama nafuu na kuwa na ushindani mkubwa sokoni na masoko kuyakamata vilivyo na hatimaye uchumi wote utahamia kwa Waislamu. Kila mmoja mmoja anaweza akajiandaa leo kupambana na vita ya Dajjal huyu wa riba ili kesho ikifika aweze kupambana vizuri. Tumuombe Allah daima Atusaidie Msaada wake ili kutufanya kuwa wenye nguvu dhidi ya biashara ya riba, riba ambayo imeingia kwenye mishipa ya damu ya shughuli zetu takribani zote, hakika Msaada wa Allah ndio Wenye kuhitajika zaidi katika zama hizi. Eeh Mola wetu tupokelee dua zetu. Amin

Wafanya Maadhimisho



Kutoka uk. 1

ya Mkuu wa Wilaya Mh. Jabiri Omari Makame.

Baada ya kurejea, wale waliokidh vigezo vya kujitolea damu miongoni mwa Khuddam waliichangia Taasisi ya Damu Salama ambayo ilipiga kambi nje ya Masjid Salaam kwa lengo hilo ambapo chupa 54 za damu zilipatikana. Ansarullah 4 pia walijihudhurisha katika uchangiaji huo.

Akiongea kwa ufupi katika hitimisho la tukio Sadr sahib MKAT aliwashukuru Khuddam na Atfal kwa kushiriki tukio na kwa nidhamu nzuri waliyoionyesha. Amir sahib aliwasifu Khuddamul Ahmadiyya kwa maandalizi mazuri ya tukio, na kwa kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa Jamaat, na kwa moyo wa kujitolea unaoonyeshwa katika uchangiaji damu. Alisisitiza kwamba moyo huu uendelee hata baadaye, kwani unatangamana na kiini cha Jamaat. Mwakilishi toka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya alisifu kazi ambayo Jamaat inaifanya ya kuwaimarisha vijana wake katika kuelekea kuhudumu wananchi wenzao, na kuwa watu wa amani na manufaa kwa jamii. Tabligh na Tarbiyyat Sheikh Bakri Abedi Kaluta na mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mh. Jabiri Omari Makame.

Baada ya kurejea, wale waliokidhi vigezo vya kujitolea damu miongoni mwa Khuddam waliichangia Taasisi ya Damu Salama ambayo ilipiga kambi nje ya Masjid Salaam kwa lengo hilo ambapo chupa 54 za damu zilipatikana. Ansarullah 4 pia walijihudhurisha katika uchangiaji huo.

Akiongea kwa ufupi katika hitimisho la tukio Sadr sahib MKAT aliwashukuru Khuddam na Atfal kwa kushiriki tukio na kwa nidhamu nzuri waliyoionyesha. Amir sahib aliwasifu Khuddamul Ahmadiyya kwa maandalizi mazuri ya tukio, na kwa kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa Jamaat, na kwa moyo wa kujitolea unaoonyeshwa katika uchangiaji damu. Alisisitiza kwamba moyo huu uendelee hata baadaye, kwani unatangamana na kiini cha Jamaat. Mwakilishi toka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya alisifu kazi ambayo Jamaat inaifanya ya kuwaimarisha vijana wake katika kuelekea kuhudumu wananchi wenzao, na kuwa watu wa amani na manufaa kwa jamii.

MATUKIO KATIKA PICHA



Wahadhiri wa Upande wa Ahmadiyya wakitoa mada na kujibu maswali katika Kongamano la Amani



Wahadhiri wa Upande wa Wasabato wakitoa mada na kujibu maswali



Washiriki wa kongamano wakiuliza maswali



Sehemu ya washiriki wa Kongamano la Amani



Amir na Mbashiri Mkuu akihutubia kongamano la amani



Baadhi ya Waahmadiyya wakisalimiana na Wasbato baada ya Sala



Wasabato Wakitaliishwa baadhi ya sehemu za Msikiti

Watu Walio Bora Kabisa: Washiriki wa Badr

Inatoka uk 12

baada ya Idi na la pili mbuzi achinjwaye kama dhabihu huwa ana umri maalumu, unaotakiwa uzingatiwe. Kwa vyovyote vile kauli asemayo Mtume*saw* ya kuwa baada ya wewe haitamtoshelezea mwingine yeyote, kuhusiana na hilo safari moja swali liliulizwa katika kikao cha Hadhrat Masih Mauud*as* ya kwamba umri wa mbuzi atolewaye kama dhabihu unatakiwa uwe kiasi gani? Hapo Hadhrat Masih Mauud*as* akamwambia Hadhrat Khalifa tul Masih Al Awwal*ra* aliyekuwa ameketi huko ya kwamba ajibu naye akasema ya kuwa kwa mujibu wa dhehebu la Ahli Hadithi mbuzi anatakiwa awe wa miaka miwili". Huzur anasema, "ipo desturi nchini mwetu ya kuwa inasemekana kwamba meno yake makubwa ya mbele yawe yamejitokeza, hivyo wakati ule Mtume*saw* akamwambia Hadhrat Abu Burdah*ra* ya kwamba dhabihu yako ya mbuzi huyo wa mwaka mmoja naikubali lakini kwa siku za usoni hairuhusiwi kwa yeyote mwingine bali mbuzi anatakiwa awe amepevuka na njia hii ndiyo iliyopo katika Jumuiya au imebainishwa katika fatua yetu kama nisemavyo na Hadhrat Masih Mauud*as* pia alisema.

Kisha yupo sahaba mwingine aitwaye Hadhrat Asad bin Yaziid*ra*. Jina la baba yake lilikuwa Yazidi bin Alfakiha naye alitokana na tawi la Banu Zuraiq la kabila la Khazraj la Ansaar. Yeye alipata kushiriki pamoja na Mtume*saw* katika vita vya Badr na Uhud. Allama Ibne Isahaq badala ya kumtaja Asad ameandika jina la Saad bin Yazid miongoni mwa masahaba wa Badr. Yapo maoni tofauti juu ya jina la Hadhrat Asad bin Yazid, wapo baadhi walioeleza jina lake kama Saad bin Zaid au Said bin Alfakiha na Saad bin Yazid.

Kisha yupo sahaba mmoja wa Badr aitwaye Hadhrat Tamim bin Ya'aar Ansari. Jina la baba yake lilikuwa Ya'aar naye alitokana na tawi la Banu Jidara bin Auf bin Alhaarith la kabila la Khajraj la Ansaar. Yeye alikuwa pamoja na Mtume*saw* katika vita vya Badr na Uhud. Hadhrat Tamim alikuwa na kijana mmoja aitwaye Ribii na binti mmoja Jamila. Mama yake alikuwa miongoni mwa kabila la Banu Ammr.

Kisha sahaba atajwaye ni Hadhrat Aus bin Thaabit bin Munzir*ra*. Huyo pia alitokana na Maansaar na kuniya yake ilikuwa Abu Shaddaad. Jina la baba yake lilikuwa Thaabit na mama yake alikuwa anaitwa Sukhtaa binti Haaritha. Yeye alikuwa baba wa sahaba mmoja maarufu sana Hadhrat Shaddaad bin Aus. Yeye alitokana na kabila la Banu Ammr bin Maalik bin Najjaar la Ansaar naye alishiriki katika baiti ya Uqba Thania na kusilimu vilevile. Akashiriki pamoja na Mtume*saw* katika vita vya Badr na Uhud. Hadhrat Hassaan bin Thabit*ra* (mshairi maarufu) na Hadhrat Ubai bin Thabit*ra* walikuwa ndugu zake. Hadhrat Uthman bin Affaan*ra* alipohamia Madina basi akakaa kwake na Mtume*saw* akafanya udugu kati yake Hadhrat Uthman bin Affaan na Hadhrat Aus bin Thaabit*ra*. Kuhusiana na kifo chake Abdullah bin Muhammad bin Ummara Ansari anasema ya kuwa kifo chake kilikuwa kimetokea katika vita vya Uhud, wapo wanaompinga pia lakini wanaohitilafiana naye ni wasimulizi dhaifu.

Kisha sahaba atakayetajwa ni Hadhrat Thabit bin Khansaa*ra*. Yeye alitokana na kabila la Banu Ghanam bin Adi bin Najjaar na akabahatika kushiriki katika vita vya Badr. Kumhusu sahaba huyo maelezo yapatikanayo na hayo tu.

Kisha alikwepo sahaba mmoja wa Badr aitwaye Hadhrat Aus bin Aswamit*ra* aliyeshiriki vita vya Badr. Hadhrat Aus bin Aswamit*ra* alikuwa ndugu yake Hadhrat Ubada bin Aswamit*ra*. Hadhrat Aus alibahatika kushiriki pamoja na Mtume*saw* katika vita vya Badr, Uhud na vita vingine vyote. Mtume*saw* aliunganisha udugu baina ya Hadhrat Aus bin Swamit na Hadhrat Marthad bin Abi Marthad Alghanawi. Imesimuliwa katika riwaya mbalimbali ya kuwa Hadhrat Aus alikuwa amemfanyia dhihaar mkewe Khuwaila binti Maalik.

Dhihaar ni ile desturi iliyokwepo miongoni mwa Waarabu ya kutengana na mke kama akimwambia kuwa yu mama yake au dada yake na hivyo walikuwa wanawaharamisha juu yao yaani wewe ni kama mama yangu hivyo umekuwa haramu kwangu. Uislamu uliifutilia mbali desturi hiyo na kutoa amri ya kuwa kutokana na tamko la kauli hiyo talaka haitokei isipokuwa hili ni jambo baya ambalo Uislamu umeweka kafara kama adhabu yake. Hadhrat Aus hakulipa kafara na kabla hajalipa kafara aliingiliana na mkewe hapo Mtume*saw* akamwamrisha akisema kuwa hayo si sahihi. Hivyo awalishe maskini sitini na hiyo ni kafara yako. Kuhusiana na Dhihaar kurani Tukufu pia imeeleza hivi: Allah Anasema; "Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama, wao si mama zao. Mama zao sio ila ni wale waliowazaa. Na kwa yakini hao wanasema maneno mabaya na uwongo; na hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye kughofiri.

Na wale wawaitao wake zao mama, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana; hayo ndiyo mnaagizwa kwayo; na Allah Anayajua mnayoyatenda.

Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza, basi awalishe maskini sitini; mmeambiwa hayo ili mumwamini Allah na Mtume Wake; na hiyo ni mipaka ya Allah; na kwa makafiri iko adhabu iumizayo. (AL-MUJAADILA 3-5)

Hadhrat Masih Mauud*as* pia ametafsiri aya hizo akisema: "Mtu akitamka mkewe kuwa mama basi kwa hakika yeye hawezi kuwa mama yake. Mama zao ni wale wale tu ambao wamezaliwa kwao hivyo jambo lao hili halina maana na ni uongo kabisa na Allah ni Msamehevu, Mwenye kughofiri, na watu wakikosea kuwaita mama kisha wakapenda kurejea kwao basi wamwachie huru mtumwa mmoja kabla ya kugusana hiyo ndiyo nasaha itokayo kwa Mungu Mwenye kujua na endapo washindwe kupata mtumwa basi wafunge saumu kwa miezi miwili kabla ya kugusana na wasioweza basi wawalishe maskini sitini"

Imesimuliwa na mkewe Hadhrat Khuwaila binti Malik bin Tha'laba ya kwamba mume wangu Aus bin Swamit alinifanyia dhihaar basi nikamwendea Mtume*saw* na kumshitaki mume wangu kwa Mtume*saw* hapo akaniambia kuwa: "Uwe mcha Mungu, yeye ni ndugu yako upande wa baba yako mdogo" ilhali nikaendelea kuweka msisitizo juu ya jambo langu mpaka aya hii ya kurani ikateremka yaani Allah Amekwisha sikia kauli ya mwanamke yule aliyejadiliana nawe kuhusiana na mumewe. (Almujadala 2)

Mtukufu Mtume*saw* akasema; "huyu yaani mumeo amwachie huru mtumwa na sasa adhabu yake ni hii ielezwayo kwenye aya kama ilivyoamrishwa na Kurani Tukufu na baadaye yapo maelezo yote yabainishwayo hapo kabla ya kuwa mwacheni mtumwa mmoja kuwa huru. Yeye anasema; "Hapo nikamweleza Mtume*saw* ya kuwa yeye hana uwezo wa hilo, ni mtu maskini" Mtume*saw* akasema basi afunge saumu kwa miezi miwili mfululizo nami nikasema ewe Mtume wa Mungu kutokana na umri wake hawezi kufunga saumu kwa miezi miwili mfululizo, hana uwezo wa hilo. Hapo Mtume*saw* akasema basi awalishe maskini sitini hapo nikasema ya kwamba yeye hana mali yoyote, hana chochote cha kutoa kama sadaka. Khuwaila anasema; nilikuwa nimeketi ndipo kiroba kimoja cha tende kililetwa kwa Mtume*saw* hapo nikasema, "ewe Mjumbe wa Allah mimi nitamsaidia kwa kiroba kingine cha tende yaani nikipatiwa kiroba hicho basi naweza kumwandalia kiroba kingine. Mtume*saw* akasema; "haya nenda nacho na kwa niaba yake uwalishe maskini sitini na urudi kwa mumeo. Huzur atba alisema ya kuwa sera ya masahaba hao ielezwapo basi pamoja nayo baadhi ya masuali pia hutatuliwa tayari.

Hadhrat Ibne Abbas*ra* anasema; "Dhihaar ya kwanza iliyofanywa katika Islam yaani kumwambia mke kuwa yu mama yake ilikuwa hiyo hiyo ya Hadhrat Aus bin Swamit. Yeye alikuwa amefunga ndoa kwa binti ya baba yake mdogo na alikuwa amemfanyia dhihaar.

Kwa vyovyote vile Allah Ameweka mipaka hii na katika zama za Hadhrat Masih Mauud*as* suala hili lilikuwa limeibuka basi yeye akasema hiyo ndiyo adhabu yake. Katika zama za Khalifa wa Pili suala kama hilo likaelezwa naye akasema kuwa adhabu yake ndiyo hii isipokuwa endapo mtu ni maskini sana, hana uwezo kabisa basi afanye istighfaar na sawa na uwezo wake atoe chochote kama fidia yake. Basi Allah katika suala la kumwita mke kuwa mama au dada Ameweka mipaka yake. Wapo baadhi wanaokuwa na tabia fulani ya kuwa wakianza kubishana tu basi wanatamka maneno haya kuwa umekuwa haramu kwangu au wewe ni kama mama yangu au wewe ni fulani au wanakula kiapo nk. Haya yote ni viapo na vina adhabu yake. Ikiwa yupo asemaye haya basi adhabu yake ni ile ielezwayo na Allah ya kuwa ampe mtumwa uhuru au afunge saumu au awalishe maskini.

Hadhrat Aus bin Swamit*ra* alikuwa mshairi vilevile. Makazi yake Hadhrat Aus bin Swamit na Shaddad bin Aus Ansari yalikuwa katika Baitul Maqdas. Kifo chake kilitokea mnamo mwaka 34 Hijria katika eneo la Ramla lililopo nchini Palestina, muda ule umri wake ulikuwa miaka 72.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JAM. II-RAJAB 1439 AH | MACHI 2019 | AMMAN 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allahsaw. alisema: Mtu afapo amali zake hukoma isipokuwa mambo matatu: Sadaka ya kudumu, elimu wanayofaidika nayo wengine au mtoto mwema anayemwombea yeye (mzazi marehemu) (Muslim)

Watu Walio Bora Kabisa: Washiriki wa Badr

Katika hotuba ya 8/2/2019, baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah,Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba)alisema:

Leo Masahaba nitakaowazungumzia, miongoni mwao jina la kwanza ni la Hadhrat Abu Mulail bin Al Azar. Jina la mama yake lilikuwa Ummi Ammr binti Ashraf naye alitokana na kabila la Aus la Ansaar. Yeye alibahatika kushiriki katika vita vya Badr na Uhud. Kutokana na riwaya moja ndugu yake Hadhrat Abu Habib bin Azar pia alikuwa ameshiriki katika vita vya Badr na vita vingine.

Sahaba wa pili ni Hadhrat Anas bin Muaaz Ansarira. Katika baadhi ya riwaya jina lake Unais pia limebainishwa naye alitokana na tawi la Banu Najjaar la kabila la Khazraj la Ansaar. Jina la mama yake lilikuwa Ummi Unaas binti Khalid. Yeye alishiriki pamoja na Mtumesaw katika vita vya Badr, Uhud, Khandak na vita vingine vyote. Katika vita vya Uhud ndugu yake Hadhrat Ubai bin Muaazra pia alishiriki pamoja naye. Kuhusu kifo chake kuna hitilafu, imebainishwa katika riwaya moja ya kuwa kifo chake kilitokea katika zama za ukhalifa wa Hadhrat Uthmanra japokuwasawa na riwaya nyingine Hadhrat Anas bin Muaaz na ndugu yake Hadhrat Ubai bin Muaz waliuawa shahidi katika tukio la Bi'ir Ma'una.

Sahaba anayefuata ni Hadhrat Abu Shaikh Ubai bin Thabitra. Hadhrat Ubai bin Thabitra alitokana na tawi la Banu Adi la kabila la Khazraj. Kuniya yake ilikuwa Abu Shaikh. Kwa mujibu wa kauli moja kuniya hiyo ilikuwa ya mwanaye. Jina la mama yake lilikuwa Sukhta binti Haaritha. Hadhrat Ubai bin Thabit alikuwa ndugu yake Hadhrat Hassaan bin Thabit na Hadhrat Aus bin Thabitra. Yeye alishiriki katika vita vya Badr na Uhud na kifo chake kilitokea wakati wa tukio la Bi'ir Ma'una.

Jambo hili la kushiriki kwake katika vita vya Badr au kutokushiriki kwake lina hitilafu ndani mwake. Vipo vitabu tofauti vya historia. Ibne Ishaq anasema ya kuwa Hadhrat Ubai bin Thaabit alikuwa amefariki dunia katika



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London nchini Uingereza ambapo hotuba yake hurushwa mubashara kupitia satelaiti duniani kote kupitia MTA.

zama za ujahili na aliyeshiriki katika vita vya Badr na Uhud alikuwa mwanaye Hadhrat Abu Shaikh bin Ubai bin Thaabitra ijapokuwa Allama Ibne Hisham amemjumuisha Hadhrat Abu Shaikh Ubai bin Thaabitra katika washiriki wa Badr. Kuhusiana na kifo cha Hadhrat Ubai bin Thaabit imebainishwa kwenye riwaya ya kwamba yeye alifariki dunia siku lilipotokea tukio la Bi'ir Ma'una lakini riwaya zingine zinaeleza kuwa kifo chake kilitokea siku ya vita vya Uhud. Kwa vyovyote vile kwa kupitia masimulizi tunapata kuelewa kuwa sahaba aliyeuawa shahidi siku ya Uhud alikuwa si yeye bali alikuwa ndugu yake aitwaye Hadhrat Aus bin Thaabitra.

Kisha kuna kumbukumbu nyingine ya Hadhrat Abu Burdah bin Niyaarra. Kuniya yake ilikuwa Abu Burdah yaani alikuwa maarufu kwa sababu ya kuniya yake ingawaje jina lake lilikuwa Hani. Katika riwaya moja jina lake lielezwalo ni Haarith na katika riwaya nyingine jina lake limeelezwa kama Malik. Yeye alitokana na familia ya Balii ya kabila la Banu Qudhaa. Hadhrat Abu Burdah alikuwa mjomba wa Hadhrat Baraa bin Aazibra. Imebainishwa katika riwaya moja ya kuwa Hadhrat Abu Burdahra alikuwa baba mdogo wa Hadhrat Baraa bin Aazibra. Alishiriki katika baiati Uqba Thania pamwe na hayo alipata kushiriki pamoja na Mtumesaw katika vita vya Badr, Uhud, Khandak na vita vingine vyote. Siku ya ushindi wa Makka bendera ya Banu Haaritha ilikuwa mkononi mwa Hadhrat Abu Burdahra.

Abu Abas na Hadhrat Abu Burdah waliposilimu basi wakati huo wote wawili kwa pamoja walivunja masanamu ya kabila la Banu Haaritha yaani walikuwa wameyavunja masanamu yaliyokuwa ya kabila lao. Imesimuliwa na Hadhrat Abu Umama ya kuwa wakati Mtukufu Mtumesaw alipoamua kuelekea eneo la Badr kwa ajili ya vita vya Badr basi Hadhrat Abu Umama pia akawa tayari kuungana naye hapo mjomba wake Hadhrat Abu Burdah bin Niyaarra alimwambia: "Wewe ubaki ili uweze kumtumikia mama yako"mama yake alikuwa anaumwa hivyo akamwambia abaki. Hadhrat Abu Umama akasema, naye alikuwa na jazba jinsi Uislamu ulivyokuwa ukishambuliwa hivyo alikuwa ana tamani kushiriki vilevile, hivyo akamwambia ya kwamba huyo ni dada yako pia. Wewe unaniambia, sasa wewe ubaki. Wakati jambo hilo lilipoelezwa mbele ya Mtumesaw basi Mtumesaw akamwamrisha Hadhrat Abu Umama abaki yaani mwanaye na Hadhrat Abu Burdah akafuatana na jeshi. Mtukufu Mtumesaw aliporudi kutoka vitani wakati huo mama yake Hadhrat Abu Umama alikuwa amekwishafariki dunia. Mtukufu Mtumesaw alisali sala yake ya jeneza.

Siku ya vita vya Uhud Waislamu walikuwa na farasi wawili. Mmoja wao alikuwa kwa Mtumesaw ambaye jina lake lilikuwa Assakab na farasi wa pili alikuwa kwa Hadhrat Abu Burdah aliyekuwa akiitwa Mulawih.

Hadhrat Abu Burdah bin Niyaarra anasimulia: "Mtukufu Mtumesaw alienda kuwatembelea baadhi ya makabila na kuwaombea lakini akaliacha kabila moja na hakulitembelea hapo watu wa kabila lile wakajisikia vibaya ya kuwa sababu yake ni ipi? Hapo wakachunguza mali ya mwenzao ndipo wakaukuta mkufu mmoja kwenye shuka lake ambao alikuwa ameuchukua akifanya hiyana kisha wakaurudisha mkufu ule basi Mtumesaw akaenda kwao na kuwaombea vilevile.

Hadhrat Abu Burdahra alishiriki pamoja na Hadhrat Alira katika vita vyote. Kifo chake kilitokea mwanzoni mwa zama za Hadhrat Muaawiara. Zipo riwaya tofauti za mwaka wa kufariki kwake,sawa na riwaya moja kifo chake kilitokea mnamo mwaka 41 wa Hijriya ijapokuwa katika riwaya zingine mwaka wa 42 Hijriya na mwaka wa 45 Hijriya pia umetajwa.

Hadhrat Baraa bin Aazibra anasimulia; "Mtukufu Mtumesaw siku ya Idi kubwa baada ya sala alituhutubia na kusema; "yeyote asaliye kama tusalivyo na kuchinja dhabihu jinsi tuchinjavyo basi yeye alifanya vizuri lakini aliyechinja kabla ya sala basi mbuzi yule atakuwa kwa ajili ya nyama tu yaani hatakuwa dhabihu bali kuchinja kabla ya sala ya idi ni kama kuchinja kwa ajili ya kula nyama." Hapo Hadhrat Abu Burdahra akasimama na kusema, "ewe Mtume wa Mungu! mimi nimechinja kabla sijatoka kwa ajili ya sala nami nilifikiri ya kuwa siku ya leo ni siku ya kula na kunywa hivyo nikafanya haraka, nikala na pia nikawalisha wanafamilia yangu na majirani. Mtumesaw akasema, "mbuzi huyo amechinjwa kwa ajili ya nyama tu, hii siyo dhabihu yako". Hapo Hadhrat Abu Burdahra akasema, "ninao mbuzi wawili jike wa mwaka mmoja nao ni bora kuliko mbuzi wawili wachinjwao kwa ajili ya nyama yaani wamenenepa mno ingawaje ni wa mwaka mmoja lakini ni bora kuliko mbuzi wawili, ikiwa niwachinje kama dhabihu basi je hiyo itanitosheleza"? Mtukufu Mtumesaw akasema, "sawa chinja tu lakini baada yako haitamtoshelezea yeyote mwingine, wewe una ruhusa tu lakini hakuna mwingine atakayeruhusiwa baada yako.

Hadithi zingine pia zinafafanua ya kuwa dhabihu achinjwe